JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA KUZUIA UENDELEZAJI, UZALISHAJI, ULIMBIKIZAJI WA SILAHA ZA KIBAIOLOJIA NA SUMU PAMOJA NA UANGAMIZAJI WAKE WA MWAKA 1972

(THE CONVENTION ON PROHIBITION OF DEVELOPMENT, PRODUCTION AND STOCKPILING OF BACTERIOLOGICAL (BIOLOGICAL) AND TOXIN WEAPONS AND ON THEIR DESTRUCTION, 1972)

NOVEMBA, 2018

YALIYOMO

1.0 **UTANGULIZI** 1

2.0 **MAPITIO YA MACHAPISHO MBALIMBALI KUHUSU MKATABA** 2

2.1 Chimbuko la dhana ya Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake 3

2.2 Jitahada za Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kibailojia na Sumu 4

2.3 Kusainiwa kwa Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake 6

2.4 Faida za kuridhia Mkataba 8

2.5 Hasara za kutoridhia Mkataba huu 9

3.0 USHAURI WA KAMATI 9

4.0 HITIMISHO 10

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA KUZUIA UENDELEZAJI, UZALISHAJI, ULIMBIKIZAJI WA SILAHA ZA KIBAIOLOJIA NA SUMU PAMOJA NA UANGAMIZAJI WAKE WA MWAKA 1972

(THE CONVENTION ON PROHIBITION OF DEVELOPMENT, PRODUCTION AND STOCKPILING OF BACTERIOLOGICAL (BIOLOGICAL) AND TOXIN WEAPONS AND ON THEIR DESTRUCTION, 1972)

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake wa Mwaka 1972 (The Convention on prohibition of development, production and stockpiling of bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on their Destruction, 1972).

Mheshimiwa Spika, Nyongeza ya Nane ya Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, inazipa Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Hivyo, Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeelekeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kusimamia Wizara tatu (3) za Mambo ya Ndani ya Nchi; Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jukumu la Kikanuni kuhusu kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, jukumu hili pia ni la Kikatiba chini ya Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Novemba, 2018, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Mb, na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Mkataba wa kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake. Vilevile, Kamati ilipewa maelezo kuhusu Vipengele vyake Muhimu na faida za kuridhia Mkataba huo. Baada ya maelezo hayo, Kamati ilipata fursa ya kutafakari na kujadili kwa kina Hoja hiyo ya Serikali.

2.0 MAPITIO YA MACHAPISHO MBALIMBALI KUHUSU MKATABA

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia wajibu wa Kamati katika kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, Kamati ilipitia Machapisho mbalimbali kuhusu Mkataba huo ili kupata uelewa kuhusu dhana ya Uendelezaji, Uzalishaji na Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na sumu pamoja na Uangamizaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipitia maandiko kuhusu jitihada zilizofanywa Kimataifa katika kuhakikisha udhibiti wa matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu ikiwemo kusainiwa kwa Mkataba wa Silaha za Kibailolojia. Aidha, Kamati ilijiridhisha kuhusu tarehe ambayo Tanzania ilisaini mkataba huo, Idadi ya nchi zilizosaini, Idadi na Nchi zilizokwisharidhia pamoja na Idadi na Nchi ambazo hazijasaini wala kuridhia. Aidha, Kamati ilijiridhisha kuhusu faida zitakazopatikana kutokana na Tanzania kuridhia Mkataba huo na hasara zinazoweza kupatikana kwa kutouridhia Mkataba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Machapisho mbalimbali kama ilivyoelezwa hapo juu, Kamati ilibaini yafuatayo:-

2.1 Chimbuko la dhana ya Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake

Mheshimiwa Spika, Silaha za Kibaiolojia zilitambulika rasmi kuwa moja kati ya silaha za maangamizi ya halaiki (Weapons of Mass Destruction- WMD) baada ya Marekani kushambulia Miji ya Hiroshima na Nagasaki kwa mabomu ya atomiki yaliyotengenezwa kwa urani (uranium), mwezi Agosti, 1945 [1]. Silaha hizo za Kibaiolojia hutumika kusambaza kwa makusudi magonjwa kwa binadamu, Wanyama na mimea kupitia vimelea (virusi, bakteria, au fangasi) kwa lengo la kusababisha madhara makubwa na wakati mwingine vifo na uharibifu wa uoto wa asili na mimea kwa 'adui' ambaye hajajipanga kabisa kuvamiwa kwa njia hiyo. Vimelea hivyo husambazwa kwa kupitia hewa, maji, vyakula, Wanyama, mimea na wadudu.

Mheshimiwa Spika, Kumbukumbu zinaonesha kuwa silaha za kibailojia zilianza kutengenezwa na kutumika tangu miaka ya 1346 ambapo matukio mbalimbali yamerekodiwa ikiwa ni pamoja na Uingereza kugawa mablanketi yenye virusi vya tetekuwanga kwa wananchi wa India wakati wa vita kati ya India na Ufaransa mwaka 1767; na Japan kusambaza bacteria wa homa ya tumbo kwenye hifadhi kuu ya maji yanayotumiwa na Jeshi la Shirikisho la Kisovieti mpakani mwa Mongolia mwaka 1939.

[1] Croddy and Wirtz, Weapons of Mass Destruction, An Encyclopaedia of Worldwide policy, Technology and History, 2005

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa vimelea vitumikavyo kama silaha za kibaiolojia na sumu vinaweza kumilikiwa si tu na Nchi bali na watu au Taasisi binafsi wakiwemo Magaidi, jambo ambalo linaongeza uwezekano wa kutokea kwa mashumbulio ya aina hiyo katika zama hizi ambazo matukio ya ugaidi yanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madhara makubwa yatokanayo na matumizi ya silaha za kibailojia na sumu, kumekuwa na jitihada mbalimbali za kupinga matumizi ya silaha hizo kupitia Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Shirikisho la Kimataifa (League of Nations) na Umoja wa Mataifa (United Nations) kama inavyoelezwa hapa chini.

2.2 Jitahada za Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kibailojia na Sumu

Mheshimiwa Spika, Jitihada za kuzuia uzalishaji na matumizi ya silaha za kibailojia na sumu zinaonekana kuanzia kwenye Mikataba ya *The Hague* ya Mwaka 1899 na 1907 maarufu kama *The Hague Conventions/ The Hague Peace conferences of 1899, 1907*[2]. Mikataba hii ndio iliyokuwa ya kwanza kutambua uhalifu wa kivita (war crimes) katika Sheria za Kimataifa. Mikataba hii, pamoja na mambo mengine, iliweka taratibu za uendeshaji wa vita ikiwa ni pamoja na kulinda Raia na mali zao wakati wa vita, kwa kuzingatia *liaber code*[3]. Hata hivyo, Mikataba hiyo haikuainisha udhibiti wa silaha ikiwemo silaha za kibaiolojia na sumu wakati wa vita

[2] United Nations Institute of Disarmament Research (UNIDIR), The Role and importance of the Hague conferences: A historical Perspective available at www.unidir.org

[3] Lieber code of April 1863, was an instruction signed by US President Abraham Lincoln during American Civil War that dictated how soldiers should conduct themselves in wartime.

ingawa ilifanikiwa kuweka mifumo ya kitaasisi ya kutatua migogoro ya kimataifa kwa amani[4] .

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa mikataba hiyo haikuainisha udhibiti wa matumizi ya silaha za kibailojia, Shirikisho la Kimataifa, mnamo tarehe 17 June, 1925 lilipitisha Itifaki ya Geneva (Geneva Protocol) ya Kuzuia matumizi ya Silaha za kibaiolojia na Sumu katika vita baina ya Mataifa (The Protocol for the prohibition of the use in War Asphyxiating, Poisonous or other Gases and of Bacteriological methods of Warfare). Itifaki hii ilianza kutumika tarehe 8 Februari, 1928 kabla ya Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, Itifaki hii haikuzuia uendelezaji, uzalishaji na ulimbikizaji wa silaha za kibaiolojia na Sumu[5].

Hivyo, kutokana na upungufu huo, tarehe 10 Aprili, 1972, Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (The Convention on prohibition of development, production and stockpiling of bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on their Destruction) unaojulikana kama *the Biological Weapons Convention*[6] (BWC). Mkataba huu unakataza kabisa uendelezaji, uzalishaji na ulimbikizaji wa silaha hizo isipokuwa kwa matumizi salama hususan kinga au dawa.[7]

[4] United Nations Institute of Disarmament Research (UNIDIR), The Role and importance of the Hague conferences: A historical Perspective, available at www.unidir.org
[5] United Nations Office for Disarmament Affairs, Biological Weapons available at www.un.org
[6] United Nations Office for Disarmament Affairs, Biological Weapons available at www.un.org
[7] Reaching critical Will, Biological Weapons, available at www.reachingcriticalwill.org

Mheshimiwa Spika, Kabla ya Rasimu ya Mkataba huo kuridhiwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN General Assembly)
mwaka 1972, baadhi ya nchi zilipinga kuwepo kwa Mkataba unaojitegemea kuhusu Silaha za kibaiolojia pendekezo lilitolewa na Shirikisho la Kisovieti kwa niaba ya nchi saba za kundi la kijamaa[8] . Hata hivyo baada ya mjadala mrefu, Marekani na Shirikisho la Kisovieti waliwasilisha mapendekezo tofauti lakini yenye maudhui yanayofanana kuhusu udhibiti wa silaha za kibaiolojia kwenye Mkutano wa *Disarmament Committee* ya Umoja wa Mataifa. Kamati hiyo iliridhia mapendekezo hayo na kuyawasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambao uridhia rasimu ya Mkataba huo tarehe 16 Disemba, 1971.

2.3 Kusainiwa kwa Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuhusu muda/ kipindi ambacho Mkataba huu ulisainiwa. Kamati ilibaini kuwa Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (The Convention on prohibition of development, production and stockpiling of bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on their Destruction) ulisainiwa tarehe 10 Aprili, 1972 na kuanza kutumika rasmi tarehe 26 Machi, 1975 ambapo hadi kufikia Mwezi Septemba 2018, nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa 182 zilikuwa zimeridhia.

[8] United Nations: The Biological Weapons Convention: An introduction, 2017

Aidha Kamati ilibaini kuwa ni nchi 10 tu za Umoja wa Mataifa ambazo hazijasaini Mkataba huo[9]

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilisaini Mkataba huo tarehe 12 Agosti, 1972 Jijini London, Uingereza ikiwa ni **miaka 46 iliyopita** na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi tano (5) ambazo zilisaini Mkataba huo lakini hadi sasa hazijauridhia. Nchi hizo ni pamoja na Haiti, Misri, Somalia na Syria ambazo baadhi yake zimekuwa na matatizo ya kivita ikilinganishwa na Tanzania, jambo ambalo linaweza kuifanya Tanzania kudhaniwa kuwa haina sababu ya msingi ya kutouridhia Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa zipo nchi ambazo hazikusaini Mkataba huo lakini zilijiunga baadae na kuuridhia Mkataba huo (Accession/ Ratification) kutokana na umuhimu wake. Nchi hizo ni pamoja na Jamaica- 1975, Kenya 1976, Libya- 1982, Burkina Faso na Swaziland 1991, Albania na Uganda 1992, na Croatia na Estonia 1993[10].

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu msingi wa Tanzania kuchelewa kuridhia Mkataba huo. Kwa sababu hio, Serikali ilitoa maelezo kuwa, ucheleweshwaji huo unatokana na nia njema ya Serikali ya kujiridhisha kuhusu umuhimu wa kuridhia Mkataba. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, awali Mkataba huu ulikuwa ukitiliwa mashaka kuwa unawanufaisha Mataifa Makubwa ambayo mengi yao yameshatengeneza silaha za kibaiolojia. Serikali

[9] Chad, Comoros, Djibouti, Eritrea, Israel, Kiribati, Micronesia, Namibia, South Sudan, Tuvalu

[10] Arms Control Association, Biological Weapons Convention Signatories and State Parties, 2018 Available at www.armstrong.org

iliithibitishia Kamati kuwa imejiridhisha kwamba manufaa yatakayopatika kwa kuridhia Mkataba huo ni makubwa, jambo ambalo Kamati ililiafiki.

2.4 Faida za kuridhia Mkataba

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati imebaini kuwa zipo faida ambazo Tanzania itazipata kwa kuridhia Mkataba huu. Faida hizo ni pamoja na:-

i) Kupata fursa ya kuwa Mshiriki kamili katika mijadala ya kimataifa inayohusu udhibiti na usimamizi wa matumizi ya Silaha za kibaiolojia na sumu;

ii) Kuwa sehemu ya uhamasishaji wa matumizi sahihi na salama ya silaha za kibaiolojia na sumu. Aidha, nchi yetu itaweza kubadilishana Vifaa, teknolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha za kibaolojia na sumu kwa matumizi salama;

iii) Kunufaika kwa kupata ufadhili wa fedha na kiutaalamu kutoka Mashirika ya Kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa na Umoja wa Ulaya, na Mataifa yaliyondelea kiteknolojia, mambo ambayo yataiwezesha nchi yetu kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya silaha za kibaiolojia;

iv) Kunufaika na tafiti mbalimbali za viumbe (Wanyama na mimea) udongo na mazingira zinazofanywa na nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa walioridhia Mkataba huu;

v) Kupata uwezo wa kubaini mapema matukio yanayotokana na matumizi ya silaha za kibaiolojia na sumu na viambato vyake;

vi) Kupitia Mfumo wa kubadilishana Taarifa, Tanzania itaweza kutambua vyanzo, usambaaji na jinsi ya

kujikinga na magonjwa mbalimbali yanayoweza kusababishwa na matumizi yasiyo sahihi ya silaha za kibaojia na sumu.

vii) Kupata fursa ya kuboresha maabara za uchunguzi wa bidhaa za kibaiolojia na kufikia viwango vya Kimataifa jambo ambalo litaiwezesha kupokea sampuli kwa ajili ya uchunguzi; na

viii) Kupata fursa ya kutoa taarifa kuhusu uvunjifu wa masharti ya Mkataba huu dhidi ya Nchi wanachama kupitia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

2.5 Hasara za kutoridhia Mkataba huu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuhusu hasara zinazoweza kupatikana endapo Tanzania haitaridhia Mkataba huu. Kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa silaha za kibaiolojia kutumiwa na Taasisi au watu binafsi ikiwemo magaidi katika ulimwengu wa sasa, kwa kuridhia Mkataba huu, Tanzania itaweza kupata msaada kutoka katika Mataifa wanachama wa Mkataba endapo shambulio lolote la kibaiolojia litaipata nchi yetu. Kamati ilijiridhisha kuwa, Tanzania haiwezi kupata msaada wa aina hiyo endapo hatutaridhia Mkataba huu.

3.0 USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili kwa kina hoja ya Serikali kuhusu Azimio la kuridhia Mkataba wa kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

i) Serikali ione umuhimu wa kuwasilisha Bungeni Mikataba na Itifaki zote zenye manufaa na tija kwa Taifa ambazo

zimeshainiwa ili ziweze kuridhiwa kwa ajili ya utekelezaji wake; na

ii) Serikali itumie vizuri fursa ya kuendeleza kitaaluma na kuboresha Taasisi zitakazosimamia shughuli mbalimbali za utafiti na uchunguzi na udhibiti wa bidhaa za kibaiolojia na sumu, kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 10 ya Mkataba.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii.

Aidha, napenda kuwashukuru kipekee Wajumbe wa Kamati kwa michango mizuri wakati wa kuchambua Hoja ya Serikali. Michango yao imewezesha kuikamilisha Taarifa hii kwa wakati. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

1) Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb- **MWENYEKITI**
2) Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb- **M/ MWENYEKITI**
3) Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
4) Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
5) Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
6) Mhe. Mhe. Victor Mwambalaswa, Mb
7) Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
8) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
9) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
10) Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
11) Mhe. Cosato David Chumi, Mb
12) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb

13) Mhe. Shally Joseph Raymond, Mb
14) Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
15) Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
16) Mhe. Bonna Mosses Kaluwa, Mb
17) Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
18) Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
19) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
20) Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb
21) Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
22) Mhe. Janeth Maurice Massaburi, Mb
23) Mhe. Augostino Manyanda Masele, Mb
24) Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
25) Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mb

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mhe. Jason Rweikiza, Mb na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wabunge cha *Parliamentarians for Global Action*, kwa kukubali mwaliko na kushiriki Kikao cha Kamati cha Kuchambua Hoja ya Serikali. Mchango wake umekuwa wenye tija katika kuiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wake kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Mb, Waziri wa Ulinzi na JKT kwa uwasilishaji na ufafanuzi wa kina alioutoa wakati Kamati ikichambua Mkataba huu. Aidha, nawashukuru wataalamu wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Florence Turuka ambao ufafanuzi wao umeiwezesha Kamati kuchambua na kujiridhisha kuhusu faida za kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na

Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hili na naomba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba huu kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Salum Mwinyi Rehani, Mb

MAKAMU MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO

YA NJE, ULINZI NA USALAMA

14 Novemba, 2018